# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 032 AGOSTI 2023

TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



1 SEKTA ZATAKIWA KUCHUKUA HATUA STAHIKI UWEPO WA EL NINO

2 DKT. CHANG'A AONGOZA KIKAO CHA VIONGOZI WA JOPO LA IPCC WA KANDA YA AFRIKA



3 FAHAMU ZAIDI:

HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2023



## KITAIFA

# SEKTA ZATAKIWA KUCHUKUA HATUA STAHIKI UWEPO WA EL NINO

**Dar es Salaam**

Mkurugenzi Msaidizi (Operesheni na Uratibu), Idara ya Menejimenti ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera , Bunge na Uratibu), Luteni Kanali Selestine Masalamado alizitaka sekta kuchukua hatua stahiki kipindi cha uwepo wa hali ya El Nino katika msimu wa mvua za Vuli 2023. Hayo aliyasema wakati wa Mkutano wa 22 wa Wadau wa Utabiri wa msimu wa Mvua za Vuli, ulioandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kushirikiana na Shirika la Save the Children kwa uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Uratibu wa Maafa.




“Kama alivyoeleza Kaimu Mkurugenzi Mkuu, juu ya uwepo wa hali ya El Nino, napenda kutoa msisitizo kuwa, katika majadiliano haya, ni vyema kujikita katika kufanya tathmini na kuainisha athari zinazoweza kujitokeza katika msimu huu na kuchukua hatua stahiki”. Alisisitiza Luteni Kanali Masalamado. Aidha, alitoa wito kwa wadau kutoka sekta mbalimbali kushirikiana na TMA ili kufanikisha upatikanaji wa taarifa za kisekta.

Awali, Luteni Kanali Masalamado aliipongeza Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kwa kuendelea kushirikisha wadau mbalimbali katika shughuli zao za utoaji wa huduma za hali ya hewa ambazo ni pamoja na utabiri wa misimu ya mvua. Alisema ushirikiano unaofanyika ni mfano wa kuigwa na unafaa kuendelea hasa katika kipindi hiki ambapo nchi yetu na dunia kwa ujumla inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa.



Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC) Dkt. Ladislaus Chang'a alieleza ni muhimu izingatiwe kuwa katika msimu huu wa Vuli, 2023 mifumo ya hali ya hewa ilionesha uwepo wa hali ya El Nino ambayo ilianza kujitokeza mapema mwezi Juni, 2023 na iliendelea kuimarika. Alisema"Mkutano huu ni muhimu sana kwa wadau wa hali ya hewa kupata fursa ya kujifunza kwa undani na kuongeza uelewa kuhusu matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa katika sekta mbalimbali na hivyo kuendelea kuboresha na kuongeza tija".

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Programu kutoka Shirika la Save the Children, Bw. Anatoli Rugaimukamu, alisema kikao hiki kinatoa mwelekeo wa jinsi ya kujipanga kukabiliana na maafa hususani kwa waathirika wakubwa ambao ni watoto.


TMA ilitoa rasmi utabiri wa Msimu wa Vuli 2023 uliojumuisha maoni na ushauri wa wadau kuhusiana na athari (hasi au chanya) zinazoweza kutokea kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa katika msimu huu.



## KIMATAIFA

# DKT. CHANG'A AONGOZA KIKAO CHA VIONGOZI WA JOPO LA IPCC WA KANDA YA AFRIKA

**Dodoma**




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi "Intergovernmental Panel on Climate Change (IPCC)", Dkt. Ladislaus Chang'a, aliongoza kikao cha viongozi wa Jopo hilo wanaowakilisha Kanda ya Africa.

Kikao hicho ambacho kilifanyika kwa njia ya mtandao, kilihusisha Makamu Wenyeviti wa Vikosi Kazi vya Jopo la IPCC wanaowakilisha kanda ya Afrika (Vice Chairs of IPCC Working Groups and Task orce Bureau on National Greenhouse Gas Inventories). Lengo la kikao hicho lilikuwa kuandaa mikakati ya kuwezesha kanda ya Afrika kushiriki kikamilifu katika Tathmini ya Saba ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC Seventh Assessment Cycle-AR7) kwa kuchangia ipasavyo taarifa za kitaalamu katika Taarifa ya Tathmini hiyo inayotarajiwa kuchukua miaka mitano hadi saba.

Mikakati hii ililenga pia kutatua changamoto ya muda mrefu ya uhaba

wa taarifa za kitaalamu za mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi zinazohusu Afrika katika Taarifa za Tathmini zinazoandaliwa na IPCC (IPCC Assessment reports). Taarifa hizo za kitaalamu ambazo huchangia katika maamuzi yanayofanywa kwenye mikutano ya kimataifa kuhusiana na mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi duniani, zinatokana na tafiti zinazofanywa na kuchapishwa katika majarida ya kimataifa.

Katika kutatua changamoto hiyo na kuiwezesha Afrika kushiriki kikamilifu katika Tathmini ya Saba, viongozi hao walikutana na kujadili masuala mbalimbali. Miongoni mwa masuala waliyojadili ni kuainisha vipaumbele vya Afrika katika Tathmini ya Saba ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi; kuanzisha kanzidata ya taasisi zinazofanya tafiti zinazohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi; kuanzisha kazidata yawanasayansi na wataalamu mbalimbali kutoka Afrika wanaofanya tafiti zinazohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi; kukusanya taarifa za wanasayansi wanaochipukia wanaoweza kujengewa uwezo kutoa mchango katika sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi; na kuandaa vikao vya kuwashirikisha na kuwahamasisha wataalamu na taasisi kutoa mchango kupitia tafiti Barani Afrika.

Jopo la IPCC ni Chombo cha Umoja wa Mataifa kinachosimamiwa na WMO na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (United Nations Environmental Programme- UNEP). Chombo hicho kilianzishwa kwa jikumu lakusimamia sayansi ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ambapo Jopo hilo hufanya tathmini za mwenendo wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi na kuandaa taarifa za tathmini (Climate Change Assessment Reports) ambazo ni muhimu sana katika kufanya maamuzi ili kukabiliana na madhara yanayosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

Tangu kuanzishwa kwa IPCC mwaka 1988 imeandaa taarifa sita za tathmini, ambapo tathmini ya sita (IPCC Sixth Assessment cycle) ilianza mwaka 2015 na kukamilika mwaka 2022. Dkt. Chang'a ni miongoni mwa viongozi wapya waliochaguliwa mwezi Julai, 2022 ambao watasimamia Tathmini ya Saba ya IPCC ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC Seventh Assessment Cycle - AR7) ambayo inayotarajiwa kuanza mwaka huu na kukamilika mwaka 2030.

# FAHAMU ZAIDI

## HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2023

Mwelekeo wa hali ya hewa kwa kipindi cha mwezi Septemba 2023, unaonesha kuwa maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuendelea kuwa makavu hususan wiki mbili za mwanzo, ikiambatana na ongezeko la joto kiasi. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, ukanda wa Ziwa Victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki. Kwa upande mwingine, vipindi vya upepo mkali unaofikia kasi ya km 40 hadi 50 kwa saa vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo, hususan ukanda wa pwani, kati, nyanda za juu kusini magharibi na maziwa makuu.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 21°C hadi 27°C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu, viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 16 °C na 21°C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 13°C hadi 21°C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 13°C. **Kwa ujumla hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Maeneo mengi yanatarajiwa kuwa na viwango vya joto la chini kati ya nyuzi joto 17 °C hadi 23 °C. Aidha, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 17 °C. Kwa upande mwingine, **vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan wiki ya tatu na ya nne.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 17 °C hadi 23 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu pamoja na vipindi vichache vya mvua inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 13 °C hadi 21 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 11°C hadi 18°C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe, yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi zaidi kwa viwango vya chini ya nyuzi joto 11°C. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya miinuko.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 19°C hadi 25°C katika maeneo mengi. Kiujumla hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo ya mwambao wa pwani, hususan wiki ya tatu na ya nne.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 13°C hadi 20°C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 13°C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.** |

JARIDA LA MWEZI

07 TOLEO NA. 032 AGOSTI 2023

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

# BIDHAA NA HUDUMA ZA TMA

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA KWA SEKTA AFYA

Kuanzia uchunguzi hadi usafirishaji, mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya mafuta na gesi huathiriwa na hali ya hewa. Hali mbaya ya hewa kama vile dhoruba, theluji, barafu, mawimbi ya joto na upepo mkali inaweza kuwa na athari kubwa kwenye ufanisi wa sekta hii. Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania inatoa huduma za hali ya hewa zinazosaidia sekta ya Mafuta na Gesi kudhibiti athari zinazohusiana na hali mbaya ya hewa.

### TMA inatoa huduma zifuatazo Kwa sekta ya Mafuta na Gesi

(a) Tahadhari juu ya vimbunga vya kitropiki;
(b) Utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, hali ya bahari au ziwa pamoja na utabiri wa upepo, mawimbi, joto la maji na kupwakujaa;
(c) Vifaa vya hali ya hewa kwa uchunguzi wa baharini;
(d) Tahadhari ya hali mbaya ya hewa kali ikiwemo na Tsunami;
(e) Nguvu na mwelekeo wa upepo uliopo;
(f) Urefu wa vipindi vya ukavu au mvua katika msimu;
(g) Takwimu za klamatolojia kama vile mgandamizo wa angahewa, unyevuanga, mvua, halijoto na takwimu za upepo.

### Matumizi ya Huduma zitolewazo na TMA kwa Sekta ya Mafuta na Gesi

(a) Utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi.
(b) Usafirishaji na uhifadhi wa mafuta na gesi.
(c) Kufanya maamuzi juu ya namna bora ya kulinda vyombo dhidi ya mafuriko au kuhamishiwa katika bandari nyingine kwa lengo la kupunguza uharibifu kwa watu pamoja na mali au vyombo vinavyomilikiwa na makampuni katika bandari na ukanda wa pwani.
(d) Njia na mpango mbadala wa akiba ya moja kwa moja unaotokana na upotevu wa muda na vifaa






JARIDA LA MWEZI
TOLEO NA. 029
MEI 2023
TMA
1 ELIMU YA HALI YA HEWA YATOLEWA KWA WATU WENYE UHITAJI MAALUM
2 TANZANIA YAPEWA KIPAUMBELE UBORESHAJI WA MIUNDO MBINU YA HALI YA HEWA
3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI JUNI, 2023


**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tmaservices

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline TV

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.